MIDWIFE ANITHA'S BREASTNEST
NURTURING HEALTHY BABIES, BUILDING OUR NATION

# MAMBO MUHIMU KUHUSU UNYONYESHAJI WA MAZIWA YA MAMA


- Anitha Mganga
- Mkunga/Kocha wa wanawake baada ya kujifungua/Mtaalamu wa unyonyeshaji maziwa ya mama.
- mgangaanitha@gmail.com +255713599154

# Thamini Unyonyeshaji: Weka Mazingira Wezeshi kwa Mama na Mtoto

**Kwa nini unyonyeshaji ni muhimu?**

- Hupunguza vifo vya watoto wachanga
- Hutoa kinga ya mwili dhidi ya magonjwa
- Hujenga ukaribu wa kihisia kati ya mama na mtoto
- Hupunguza hatari ya saratani ya matiti na ovari kwa mama

# Maziwa ya Mama – Chakula Bora kwa Mtoto

- ◈ Hupatikana muda wote, halihitaji maandalizi
- ◈ Hujitosheleza kwa mahitaji ya mtoto miezi 6 ya kwanza
- ◈ Huzuia magonjwa kama kuhara, pneumonia, na utapiamlo
- ◈ Hupunguza gharama za familia na mzigo wa kiafya kwa taifa

# Jinsi Maziwa Yanavyotengenezwa (Hatua 3 za Lactogenesis)

**Lactogenesis I (Wiki 16-Punde kabla ya kujifungua):**

- Matiti huanza kutengeneza colostrum (ziwa la awali lenye kinga nyingi)

**Lactogenesis II (Siku 2-3 baada ya kujifungua):**

- Kuongezeka kwa homoni ya prolactin, hupelekea "ziwa kujaa"
- Maziwa hutoka kwa wingi na kuanza kuonekana meupe au ya samawati

**Lactogenesis III (Kuendelea kwa utengenezaji wa maziwa):**

- Hufanikishwa na kunyonya mara kwa mara na kufika kwa mtoto kifuani
- Uhusiano wa mahitaji ya mtoto na utolewaji wa maziwa hujengwa

# Changamoto kwa Wakunga na Wataalamu wa Afya

**Changamoto kuu:**

- Mama kuchoka au kupata ganzi baada ya upasuaji
- Watoto waliozaliwa njiti au wenye matatizo ya kiafya
- Upungufu wa vifaa vya kufanikisha mawasiliano ya ngozi kwa ngozi
- Upungufu wa maarifa miongoni mwa baadhi ya watoa huduma
- Ukosefu wa sera rafiki kazini kwa wakunga wenye watoto

MIDWIFE ANITHA'S BREASTNEST
NURTURING HEALTHY BABIES, BUILDING OUR NATION

# Suluhisho

- Mafunzo endelevu kwa wakunga kuhusu unyonyeshaji
- Mfumo wa rufaa unaozingatia muda wa saa 1 ya kwanza
- Huduma ya kiunganishi kati ya mama na mtaalamu wa kunyonyesha
- Uboreshaji wa miundombinu ya wodi za mama na mtoto

# Wito kwa Wadau

- Tuweke Mazingira Wezeshi
- Tunaposema “mazingira wezeshi,” tunamaanisha nini?
  - Sera zinazowalinda mama kazini ili waendelee kunyonyesha
  - Upatikanaji wa huduma rafiki kwa mama (lactation support)
  - Ushirikiano kati ya familia, jamii, na wahudumu wa afya
  - Kuwekeza katika mafunzo na vifaa vya kusaidia unyonyeshaji

MIDWIFE ANITHA'S BREASTNEST

NURTURING HEALTHY BABIES, BUILDING OUR NATION

# Wito

*Tuthamini na tuweke mazingira wezeshi kwa unyonyeshaji wa maziwa ya mama sio tu kama suala la afya, bali pia kama haki ya mama na mtoto.*

*Midwife Anitha,2025.*